

JARIBIO LA KITARAFU

DARASA LA TANO MUHULA WA III 2009

KISWAHILI

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuoka 1-15

Mwanafunzi _____ 1 _____ katika darasa _____ 2 _____ tano alikuwa _____ 3 _____ mwana mbuzi kando. Kwa hivyo alikuwa na _____ 4 _____ ya _____ 5 _____ karatasi mithili ya ng'ombe anayecheua. Kwa bahati mbaya aliamua _____ 6 _____ dirisha moja. _____ 7 _____ wapi! _____ 8 _____ wa zamu alikuwa akipita karibu na darasa letu. Naye _____ 9 _____ jicho _____ 10 _____ hadi akapiga _____ 11 _____ . Muda si _____ 12 _____ alija darasani huku amependwa na _____ 13 _____ za _____ 14 _____ na kuapa _____ 5 _____ kijeshi iwapo haungemtaja mwanafunzi aliyemgonga.

A	B	C	D
1. mmoja	moja	kimoja	limoja
2. yetu	kwetu	letu	chetu
3. mkaidi	mjeuri	mtukutu	mbaya
4. madhara	mazoea	matabia	matarajio
5. kula	kumeza	kurarua	kutafunatafuna
6. kuchungufia	kuirusha	kulifungua	kuvunga
7. lakini	kwa	ole	chupi
8. kijana	mwalimu	kiranja	mtoto
9. akamtoa	akamvunja	akamzaba	akamgonga
10. moja	limoja	kimoja	lote
11. kamsa	teke	sauti	kilio
12. muda	wakati	wakaa	mfupi
13. kelele	kumuna	kukasirika	hasira
14. wazimu	mkizi	mwaka	wingi
15. kutupiga	kutuonyesha	tutalia	kutuadhibu.

Kutoka namba 16-30 jibu kuliungana na maagizo

16. **Andika ukubwa**

- Mtoto huyu ni mdogo
A. jitoto hili ni ndogo
B. kitoto hicho ni kidogo
C. toto hilo ni dogo
D. toto hili ni dogo

Majina ya makundi

17. _____ wa magari

- A. mfuatano B. mstari
C. mlolongo D. mwendo

18. Mtoto wa ng'ombe ni ndama naye wa bata huitwa

- A. shibili B. kiyoyo
C. kibata D. kipepeo

19. Makao ya binadamu ni nyumba nayo ya Raisi ni

- A. kasri B. handaki
C. ikulu D. paradiso

Kitendawili

20. Mgeni asiyependwa

- A. kifo B. mbwa
C. giza D. usingizi

Methali

21. Mkono mmoja _____ ng'ombe.

- A. huketi B. hushika
C. huchemsha D. hauchiji

22. Akisami hii huitwaje?

- A. tusui B. theluthi

C. thumni

D. thuni

Kukanusha

23. Akienda sokoni ataninunulia sukuma wiki

- A. hakuenda sokoni kuninunulia sukumawiki
B. hajaenda sokoni wala hakuninulia sukumawiki
C. kama ataenda sokoni ataninunulia sukumawiki
D. asipoenda sokoni hataninunulia sukumawiki.

24. Kula

- A. usikule B. hajala
C. usile D. hakula

25. Ndugu wa kiume wa mama yangu huitwa

- A. ami B. mjomba
C. amu D. halati

26. Mtu ambaye amepindika mgongo ni

- A. kibogoyo B. kibiongo
C. kiziwi D. kipinde

27. Neno mwalimu liko katika ngeli gani?

- A. A-I B. WA-A
C. A-WA D. KI-VI

28. Baba yangu ni simba. Hii ni fani ya lunga inayoitwa

- A. tashbihi B. istiara
C. semi D. methali

29. Kati ya mapambo haya ni gani si pambo la sikioni?

- A. bali B. kipuli
C. mapete D. kishaufu

30. Buibui ni vazi la kike hasa sana linalovaliwa na waislamu pia ni

- A. mdudu B. peremende
C. kalamu D. mfuko

Soma habari ifuatayo kisha ujibu 31-40

Usiku huo ulikuwa mrefu kuliko kawaida. Ama kwa kweli nilipata usingizi wa mang'amung'amu. Ghafula kama ajali kamsa ilipigwa. Papo hapo nikajua mambo yametumbukia nyongo. Niliwaamsha wavyele wangu. Punde si punde walienda kumpiga jeki jirani yetu aliyekua amevamiwa na wezi. Hata hivyo hawakupoteza wakati kwa sababu walianza kupambana nao. Nao walibahatika kwa kuwakamata wezi wawili.

Wanakijiji waliojaa hasira walikata kauli kuwachoma. Kufumba na kufumbua magurudumu yaliletwa pamoja na mafuta taa. Hatimaye waliwashwa moto Lo! Baba yangu alipowaangalia vizuri aligundua ndugu yangu alikuwa mmoja wao. Naye alimwonea huruma lakini angefanyaje na maji yakimwagika hayazoleki?

- | | |
|--|---|
| 31. Mwandishi alilala usingizi upi?
A. fofofo
C. mang'amung'amu
32. Ni nini ilipigwa ghafula?
A. kilio
C. ngoma
33. Maana ya mambo kutumbukia nyongo ni
A. kuharibika
C. kupongezwa
34. Kwa nini waliamka na kwenda kwa jirani?
A. wakagombane
C. watazame runinga
35. Piga jeki ni fani ya lugha inayoitwa
A. semi
C. tashbihi
36. Binadamu ni kwa miguu, magari ni kwa magurudumu na vitanda ni kwa | A. vitendaguu
C. matendeguu
B. kabisa
D. fefefe
B. sauti
D. kamsa
B. kuendelea
D. kuisha
B. wakasaidie
D. wakawacheke
B. methali
D. mafumbo
B. miguu
D. mijiguu
37. Maana kwa kufumba na kufumbua ni
A. kufunga na kufungua macho
B. kufumbua ni kinyume cha kufumba
C. muda mfupi
D. ni pambo la mwandishi
38. Ni dhahiri shahiri kuwa baba yangu alijaribu kumkanya ndugu yangu lakini aliyatia masikio yake
A. pamba
C. maharagwe
39. Mwigika mwa ni
A. tanakali
C. tashbihi
40. Kichwa kifaacho katika habari hii ni
A. usiku
C. ndugu yangu
B. Istira
D. vitenzi
B. uchafu
D. karatasi
B. wezi
D. uui |
|--|---|

Soma habari hii kisha ujibu maswali 41-50

Watoto walisimama kwenye safu zao saa mbili kamili. Watoto pamoja na waalimu wao waliimba wimbo wa taifa. Baada ya wimbo, mwalimu mkuu alisema, "Leo ni siku ya kupanda miti hapa shuleni mwetu shule zote nchini zinapanda miti leo pia. Leo tutaeleza kwa nini tunapanda miti."

Zamani hapa nchini mvua ilinyesha mara kwa mara. Siku hizi ni kidogo. Hii ni kwa sababu miti imepunguka"

Mwalimu mkuu aliendelea, "Watu wamekata miti kwa sababu ya kuchoma makaa na kupata mahali pa kulima. Baada ya kukata miti, hawakupanda mingine. Ni vizuri kupanda mingine. Ni vizuri kupanda miti miwili baada ya kukata miti mmoja. Miti hutusaidia kuvuta mvua. Miti pia huzuia mmomomonyoko wa udongo."

- | | | | |
|--|---|--|--|
| 41. Ni nani aliyetoa hotuba hiyo?
A. chifu
C. mwalimu mkuu
42. Ni shule ngapi zilizopanda miti siku hiyo?
A. shule moja
C. shule zote
43. Zamani mvua ilikuwa
A. hainyeshi
C. nyingi
44. Ni kwa nini mvua imekuwa kidogo siku hizi?
A. miti imekauka
B. iti imepungua
C. watu wamekuwa wengi
D. hakuna miti ya kupanda
45. Kwa nini watu hukata miti?
A. watu wauze
C. kulima shamba | B. mwalimu
D. mkuu wa taifa
B. shule chache
D. shule nyingi
B. imepotea
D. kidogo
B. kutengeneza dawa
D. kuchoma makaa | 46. Ni kwa nini miti imepungua nchini mwetu?
A. watu hukata na kupanda mingine
B. watu hukata na hawapandi miti mingine
C. hakuna miti ya kupanda
D. watu wamechoka kupanda miti
47. Tumeambiwa tufanye nini tunapokata miti mmoja
A. tuchome makaa
C. tunapanda miti miwili
48. Ni nini muhimu wa miti hapa nchini?
A. huleta maji
C. tunachoma makaa
49. Neno "Imepungua" ni sawa na
A. imezidi
C. imekuwa michache
50. Undongo unaweza kuchukuliwa na nini?
A. jua
C. upepo wa maji | B. tupa sue mbao.
D. tupande mmoja
B. huleta mvua
D. hulea upepo
B. imeongezeka
D. imekonda
B. maji
D. hewa |
|--|---|--|--|